

AFRICAN UNION		UNION AFRICAINE
الاتحاد الأفريقي		UNIÃO AFRICANA
UNIÓN AFRICANA		UMOJA WA AFRIKA
MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU COUR AFRICAINE DES DROITS DE L'HOMME ET DES PEUPLES S.L.P 6274 Arusha, Tanzania – Simu: +255 272 510 510 Tovuti: www.african-court.org / Barua pepe: registrar@african-court.org		

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

UFUNGUZI WA MWAKA WA MAHAKAMA MWAKA 2025, SEMINA YA MAHAKAMA NA UTOAJI WA HUKUMU KATIKA KIKAO CHA KAWAIDA CHA 76 CHA MAHAKAMA YA AFRIKA YA

HAKI ZA BINADAMU NA WATU: TAREHE 3, 4 NA 5 FEBRUARI 2025

Arusha, tarehe 22 Januari 2025: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (AfCHPR) **Jumatatu, tarehe 3 Februari 2025** itafanya Sherehe Kuu ya kuadhimisha ufunguzi wa Mwaka wake wa Mahakama mwaka 2025, chini ya kaulimbiu "*Kuendeleza Haki kupitia Fidia*".

Sherehe hiyo itafanyika katika Makao Makuu ya Mahakama hiyo jijini Arusha, Tanzania.

Kama sehemu ya shughuli za Ufunguzi wa Mwaka wa Mahakama, Mahakama itaandaa Semina ya Mahakama mnamo tarehe **4 Februari 2025**, ikiwa na kaulimbiu "*Kutoa Haki kwa Wanawake kupitia Fidia*".

Sherehe Kuu hiyo na Semina ya Mahakama itahudhuriwa na wawakilishi wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, Mahakama za Kimataifa, Kikanda na Kitaifa, vyombo vya Umoja wa Afrika vyenye mamlaka ya haki za binadamu, taasisi za kitaifa za haki za binadamu, wataalamu wa sheria na Vyama vya Wanasheria. Aidha, mashirika ya kiraia, wanataaluma, wanahabari na wadau wengine wanaohusika katika kazi ya Mahakama na kulinda haki za binadamu barani Afrika wanatarajiwa kushiriki.

Sherehe hiyo itaanza kwa msafara wa Majaji Waheshimiwa wa Mahakama ya Afrika saa 4:30 asubuhi saa za Afrika Mashariki na itatangazwa moja kwa moja kupitia majukwaa ya kidijitali ya Mahakama.

Sherehe hii Kuu pia inaashiria kuanza kwa Kikao cha Kawaida cha 76 cha Mahakama, kilichopangwa kuanza kuanzia tarehe **3 hadi 28 Februari 2025** katika Makao Makuu yake jijini Arusha, Tanzania.

Mnamo **tarehe 5 Februari 2025**, Mahakama itatoa hukumu saba (7), zilizopitishwa wakati wa Kikao chake cha Kawaida cha 75, kuanzia saa 4:00 asubuhi saa za Afrika Mashariki.

Sherehe Kuu, Semina ya Mahakama na Utoaji wa Hukumu, shughuli hizi zitaendeshwa kwa njia mseto, ikiwapa fursa washiriki kufuatilia matukio ana kwa ana au kwa njia ya mtandao kupitia viungo vya intaneti vifuatavyo:

Chaneli ya YouTube

Chaneli ya Kiingereza: <https://www.youtube.com/c/AfricanCourtEnglishChannel>

Chaneli ya Kifaransa: <https://www.youtube.com/@courafricaine>

Chaneli ya Kiswahili: <https://www.youtube.com/@MahakamaYaAfrika>

Tovuti ya Zoom

<https://zoom.us/j/99379810510>

Msimbo siri: 379168

Kwa majukwaa yote, kutakuwa na ukalimani sambamba katika lugha za Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa, Kireno na Kiswahili.

MAELEZO KWA WAHARIRI:

1. Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (AfCHPR) ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha haki za binadamu na watu barani Afrika zinalindwa. Mahakama hii ni chombo cha Umoja wa Afrika na inakamilisha na kuimarisha kazi za Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ambayo makao yake ni Banjul, Gambia.
 2. Mahakama inaundwa na Majaji kumi na mmoja, raia wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika waliochaguliwa kulingana na uwezo wao binafsi. Mahakama inakutana mara nne kwa mwaka katika Vikao vya Kawaida na inaweza kufanya Vikao Visivyo vya Kawaida.
 3. Kila mwaka, Mahakama inazindua shughuli zake kwa sherehe kuu kuashiria ufunguzi rasmi wa mwaka wake wa mahakama, ikionyesha kujizatiti kwake katika kulinda haki za binadamu na watu kote Afrika na kwingineko. Ufunguzi huu unaonesha yale yatakayofanyika mwaka mzima na hutumika kama sehemu ya kutoa wito wa kuchukua hatua muhimu katika kulinda haki za msingi za Waafrika wote.
-

Maelezo zaidi kuhusu Mahakama yanaweza kupatikana kwenye www.african-court.org

Kwa maswali zaidi wasiliana na: Dk Robert Eno, Msajili – Robert.Eno@african-court.org

Kwa maswali kutoka vyombo vya habari wasiliana na: Chipiliro Kansilanga, Afisa Mwandamizi
wa Habari na Mawasiliano

(Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano) Chipiliro.Kansilanga@african-court.org au

AfricanCourtMedia@african-court.org